# TAARIFA KWA UMMA

## MWALIKO WA KUSHIRIKI KATIKA MAONESHO YA BIASHARA YA KIMATAIFA NCHINI ESWATINI, 2023

**Dar es Salaam - Tarehe 8 Mei, 2023**

TanTrade kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) inapenda kuwatangazia Wafanyabiashara na wawekezaji wote kuwa Mamlaka ya Uhamasishaji Uwekezaji ya Eswatini (*Eswatini Investment Promotion Authority - EIPA*) inaandaa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa yatakayofanyika katika Kituo cha Biashara na Maonesho cha Mavuso (Mavuso Trade and Exhibition Centre) kuanzia tarehe 1 hadi 10 Septemba, 2023.

Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Eswatini ni miongoni mwa maonesho makubwa ya kibiashara yanayofanyika katika Falme ya Eswatini ambapo hivi sasa yamerudi kwa kasi kubwa. Maonesho haya ya Kimataifa yamekuwa yakitoa fursa kwa washiriki kutoka katika Kanda, Mabara na Dunia kwa ujumla kuonesha bidhaa na huduma mbalimbali zinazotolewa na makampuni kutoka huko. Aidha, maonesho haya yamekuwa yakitoa fursa kwa washiriki na wageni mbalimbali kukutana na kubadilishana uzoefu katika Nyanja mbalimbali.

Wawekezaji kutoka sekta ya Viwanda, Kilimo, Miundombinu, Nishati, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Afya, Elimu na Utalii zifuatazo wanaalikwa kushiriki.

Kwa taarifa zaidi kuhusu Maonesho haya tafadhali wasiliana na Maafisa wafiuatao kutoka TanTrade: **Ms. Doroth Urio** kupitia +255 764 380 095, au **Ms. Samia Mohamed** kupitia +255 653 009695.

Imetolewa na:

Daniel J Diah

Afisa Uhusiano, TanTrade